

**HOTUBA YA MHESHIMIWA CHARLES MAKONGORO  
NYERERE MKUU WA MKOA WA RUKWA WAKATI  
ALIPOFUNGUA SEMINA YA UELIMISHAJI UMMA KUHUSU  
MAANDALIZI YA DIRA YA TAIFA YA MAENDELEO 2050  
KATIKA MKOA WA RUKWA TAREHE 22 JULAI 2023.**

- *Katibu Tawala Mkoa wa Rukwa,*
- *Ndugu Katibu wa CCM Mkoa,*
- *Kamati ya Usalama Mkoa,*
- *Wakuu wa Wilaya,*
- *Wakuu wa Seksheni na Vitengo Sekretarieti ya Mkoa,*
- *Wakuu wa Taasisi za Umma,*
- *Makatibu Tawala wa Wilaya,*
- *Wakurugenzi wa Halmashauri,*
- *Viongozi wa Dini na Vyama vya Siasa,*
- *Wawakilishi wa makundi,*
- *Wajumbe wa timu ya uandishi wa Dira 2050,*
- *Waandishi wa Habari,*
- *Wageni Waalikwa,*
- *Mabibi na Mabwana.*

**Nawasalimu kwa Jina la Jamhuri ya Muungano wa  
Tanzania.....**

Awali ya yote napenda kutumia fursa hii kumshukuru  
Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutujalia afya njema

na kutuwezesha kukutana mahali hapa tukiwa wazima na wenye afya njema. Vile vile, nitumie fursa hii kuwashukuru kwa dhati kwa mwitikio wenu wa kuhudhuria warsha hii muhimu kwa maendeleo ya Taifa letu. Kwa ujumla, tunatambua kuwa Serikali, wananchi na wadau wote wa maendeleo tupo katika maandalizi ya Dira Mpya ya maendeleo itakayobeba maono ya watanzania ifikapo mwaka 2050.

***Ndugu Washiriki,*** Semina hii inalenga kutoa elimu kwa viongozi na wawakilishi wa makundi ya wadau kuhusu Dira 2025 na utekelezaji wake pamoja na mchakato wa maandalizi ya Dira 2050. Ni imani yangu kwamba zoezi hili litasaidia kujenga uelewa kwa Viongozi wote wa Mkoa, Wilaya na Halmashauri kuhusu mchakato wa maandalizi ya dira ya maendeleo ya 2050. Hivyo mnapaswa kushiriki kikamilifu katika warsha hii kwa lengo la kuwa na uelewa wa pamoja na kuelewa majukumu yenu ya msingi ili kufanikisha shughuli hii muhimu kwa maendeleo ya Taifa letu.

***Ndugu Washiriki,*** Aidha, kwa kuwa Dira ya Taifa ya Maendeleo inagusa makundi yote, ninatarajia kutakuwa na ushirikishwaji mpana wa wadau wote katika ngazi zote ikiwemo taasisi za elimu ya juu na za utafiti, Sekta Binafsi na Asasi za Kiraia (AZAKI) na wananchi mmoja mmoja. Ushirikishwaji wa wadau utawezesha kupata Dira jumuishi yenye kukidhi mahitaji

stahiki ya Taifa katika kipindi cha miaka 25 ijayo. Nimetaarifiwa kuwa katika Mkoa wetu pamoja na warsha hii wajumbe wa timu ya uandishi watasambaza nakala za vitabu vya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 (TDV 2025), vipeperushi na mabango kuhusu maandalizi ya Dira 2050, na kutembelea Vyombo vya Habari vilivyopo katika mkoa wetu. Hii itasaidia kuongeza wigo wa watu watakaofikiwa pamoja na kuacha nyenzo zitakazosaidia kuendelea na uelimishaji umma baada ya kuondoka.

***Ndugu Washiriki,*** Kupitia warsha hii mtapata muda mzuri wa kujifunza, kubadilishana uzoefu na kujadili kwa kina kuhusu maono ya Taifa letu kwa kizazi cha sasa na kijacho. Vile vile, mtaweza kujadili kwa kina na kutumia uzoefu wenu na kutoa maoni na mapendekezo kuhusu aina ya dira tunayoitaka. Vilivile mtapata uelewa zaidi kuhusu Dira ya Maendeleo na maarifa zaidi ya kutekeleza majukumu yenu kikamilifu.

***Ndugu Washiriki,*** Mnaweza kuona kama maandalizi ya Dira hii yameanza mapema ikizingatiwa kuwa Dira tunayoendelea kuitekeleza kupitia Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/2022 – 2025/2026 itafika ukomo mwaka 2025. Ninapenda kuwajulisha kuwa muda haupo upande wetu. Hii ni kutokana na kuwa maandalizi ya Dira yanakuwa hatua kwa hatua na shughuli nyingine nyingi ikiwemo kuhakikisha ushirikishwaji wa wadau unakuwa mpana.

***Ndugu Washiriki,*** Nisingependa kutumia muda mrefu kwa kuwa zoezi hili ni letu sote na wote tunapaswa kushiriki kwa kutoa maoni na mawazo yetu. Niwasihi timu ya uandishi kuzingatia kikamilifu maoni yatakayotolewa kwa kujadiliana na kukubaliana katika warsha hii. Natumaini mtakuwa timu bora hivyo kufanikisha maandalizi ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 kama ilivyopangwa. Kwa niaba ya uongozi wa Serikali katika Mkoa wetu wa Rukwa ninawatakia warsha njema na utekelezaji mwema wa majukumu yenu.

***Baada ya kusema hayo, napenda kutamka kuwa semina ya uelimishaji umma kuhusu maandalizi ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 katika Mkoa wetu wa Rukwa IMEFUNGULIWA RASMI.***

***Mungu Ibariki Tanzania,  
Mungu Bariki Mkoa wetu wa Rukwa,***

**AHSANTENI KWA KUNISIKILIZA**

**Charles Makongoro Nyerere,  
Mkuu wa Mkoa wa Rukwa.**